OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA.

SHULE YA SEKONDARI LUANA,

S. L. P 23.

LUDEWA.

SIMU:0757 077 998

MWANAFUNZI .....
SHULE YA MSINGI .....
LUDEWA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI LUANA MWAKA 2021.

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechanguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

1.1. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, wewe unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** ukiwa na mahitaji yafuatayo muhimu ya shule.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare ya shule

(a) Suruali rangi dark blue na shati nyeupe mikono mirefu kwa wavulana.
(b) Suruali rangi dark blue na kigauni kifupi (kisolo) kwa wasichana shingo fupi
(c) Viatu rangi nyeusi vya kufungwa na kamba kwa wote na soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.
(d) Sweta rangi ya bendere ya Taifa ya Tanzania kwa wote.
(e) Track nyeusi , raba, T shirt damu ya mzee kwa wote (T. shirt) zinapatikana shuleni kwa sh. 10,000/=
(f) Godoro 1 au Tsh. 10,000 kwa mwaka kama gharama za kukodi godoro kwa wanafunzi wa bweni
(g) Sketi nyeusi yenye marinda kwa wanafunzi wa bweni

2.2. VIFAA VINGINE VYA SHULE

(a) Daftari kubwa zisizo pungua 12 penseli na peni za kutosha.
(b) Mkebe (mathematical set)
(c) Jembe jipya lenye mpini na fyeko au panga
(d) Ndoo 2 za lita 10
(e) Fagio kwa ajili ya usafi (chelewa)

2.3. MICHANGO YA CHAKULA

(a) **Debe 10** za mahindi, **debe 3** za maharage na fedha **sh. 70,000/=** kwa wanafunzi wa bweni
(b) **Debe 5** za mahindi, **debe 2** za maharange na fedha **sh. 35,000/=** kwa wanafunzi wa kutwa
(c) Kwa wasiotumia maharage waje na fedha zenye thamani ya maharage.

NB: **-**Michango ya chakula kutolewa mara mbili (2) kwa mwaka tu wakati mtoto anapokuja kuripoti Shuleni, **Januari** na **Julai .**

- Kila mgojwa aje na vithibitisho toka kwa daktari

2.4. NYARAKA MUHIMU ZA WANAFUNZI

(a) Kila mwanfunzi anatakiwa kupimwa afya yake na kujaziwa taarifa husika hospitali ya serikali kwa kutumia **fomu na 1.**

(b) Mwanafunzi na mzazi/ mlezi wanatakiwa kujaza **fomu na.2** ya kukubali nafasi ya masomo aliyo pewa mwanafunzi.

(c) Fomu ya maelekezo binafsi ya mwanafunzi

(d) Kujaza fomu ya mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo au makosa ya jinai.

NB: Fomu namba 1 na 2 zimeambatanishwa kwa pamoja na maagizo haya .

2.5. MAHITAJI MENGINE YA KIBINADAMU

(a) Mswaki na dawa ya meno

(b) Sabuni za kufulia na kuogea

(c) Mafuta ya mgando ya kupakaa na kitana cha kuchania nywele

(d) Ndala au kandambili

(e) Taulo la kujifutia maji mwilini

(f) Mashuka 2 ya rangi ya pingi

(g) Blanketi 1

(h) Chandarua 1

(i) Mto wa kulalia

(j) Sahani, kikombe, kijiko kwa ajili ya chakula

(k) Nguo za ndani za kutosha mfano chupi

(l) Kiwi nyeusi ya viatu na blashi yake

(m) Kitambaa cha mafua (lesso)

NB: Tafadhari soma kwa makini maelekezo au maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA LUANA SEKONDARI,

.....

MWINUKA O.J

MKUU WA SHULE

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na umepewa nakala yake.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
3. Kushiriki kwa makini maandalio ya jioni (reparation)
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ua nje ya mipaka ya shule, hivyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wowote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
9. Kutunza mali za Umma
10. Kusalimia wakubwa kwa wadogo
11. Kusimama wakati wakubwa wanapita

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE

1. Wizi
2. Ausherati, na ushonga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya. Kama vile uvutaji wa bangi, kokeni, mirungi n.k
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau bendela ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba
11. kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Kuwa na simu ya mkononi

FOMU NA.1

LUDEWA DISTRICT COUNCIL

LUANA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 23,
LUDEWA.
DATE:.....

A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To the medical officer.....
.....

PART A:
Pupils name:.....age.....
Please examine the above named pupil as to her/ his physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following

1. Eye sight.....
2. Hearing.....
3. Blood pressure.....
4. Urine for sugar.....
5. Asthma.....
6. Skin disease .....
7. Neurosis.....
8. Venereal disease.....
9. Pregnancy.....
10. Other serious diseases.....

PART B- MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a government medical officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that he/ she is physically mentally fit/~~unfit~~ for a full- time schooling
2. Other Comments.....

Name.....signature.....Date.....

Designation.....Official stamp.....

FOMU NA. 2

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA
SHULE YA SEKONDARI LUANA
S. L. P 23,
LUDEWA.
TAREHE .....

HATI YA KUKUBALI NAFASI YA MASOMO SHULENI.

A: MWANAFUNZI

Mimi ..... ninakubali/ sikubali kupata elimu ya sekondari kwa nafasi niliyopata baada ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii.
Nakubali/ sikubali kutii sheria za shule kama nitakavyoelekezwa na walimu.

Jina .....sahihi ..... tarehe .....

B: MZAZI /MLEZI

Mimi ..... nakubali/ sikubali kumgharamia masomo ya elimu ya sekondari mtoto wangu .....

Jina ..... sahihi ..... tarehe .....

* Futa yasiyohusika.

SARE YA SHULE ZA SEKONDARI
WASICHANA